

HALMASHAURI YA WILAYA KILINDI

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

Simu : 027-2977306
Nukushi: 027 - 2977307
BaruaPepe: kilindic@tanga.go.tz
Unapojibu taja



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 18
SONGE - KILINDI

TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE HALMASHAURI YA WILAYA KILINDI.

TUMEPOKEA BARUA KUTOKA OFISI YA KATIBU MKUU UTUMISHI YENYE KUMB NA TG.472/535/01/A/48 YA TAREHE 14.08.2018 IKIHUSU UTHIBITI WA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA TEHAMA NA MITANDAO YA MAWASILIANO YA SERIKALI.

KATIKA BARUA HIYO YAMETOLEWA MAELEZO KUWA

KASI YA MTANDAO WA INTANETI WA SERIKALI INAPUNGUA KUTOKANA NA MATUMIZI MAKUBWA YA MITANDAO YA KIJAMII HUSUSANI INAYOPAKUA VIDEO MFANO YOU TUBE NA HIVYO KUSABABISHA WATUMISHI WENGINE WANAOTUMIA MTANDAO WA INTANETI WA SERIKALI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU RASIMI YA KISERIKALI KUATHIRIKA.

PIA BAADHI YA WATUMISHI WAMEKUWA WAKITUMIA MUDA MWINGI KWENYE MITANDAO YA KIJAMII WAKATI WA MUDA WA KAZI JAMBO AMBALO NI KINYUME NA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA UTUMISHI WA UMMA.

AIDHA MALALAMIKO HAYO PIA YAMEKUWA YAKITOLEWA NA WAMILIKI WA VIDEO, PICHA NA NYARAKA MBALIMBALI WAKITUHUMU UPAKUAJI WA NYARAKA HIZO ZENYE HATI MILIKI BILA IDHINI YAO KWA KUTUMIA MTANDAO WA INTANETI WA SERIKALI.

HIVYO KUTOKANA NA UTUMIAJI MBAYA WA INTANETI YA SERIKALI, SERIKALI IMEPANGA KUCHUKUA HATUA ZIFUATAZO KATIKA KUDHIBITI.

MITANDAO YA KIJAMII HAITAPATIKANA KUPITIA INTANETI YA SERIKALI WAKATI WA MUDA WA KAZI YAANI KUENZIA SAA 01:30 ASUBUHI MPAKA SAA 09:30 ALASIRI.

WATUMISHI WA UMMA HAWATAWEZA KUPAKUA NYARAKA, PICHA NA VIDEO ZENYE HATI MILIKI KWENYE INTANETI YA SERIKALI BILA IDHINI YA WAMILIKI WA NYARAKA HUSIKA.

HIVYO OFISI YA KATIBU MKUU UTUMISHI INAWAAGIZA WATUMISHI WOTE WA UMMA KUTEKELEZA NA KUZINGATIA MIONGOZO YOTE YA TEHAMA JUU YA MATUMIZI YA INTANETI YA SERIKALI.

NB: TAASISI ZENYE MAHITAJI MAALUMU YA MATUMIZI YA MITANDAO YA KIJAMII WAKATI WA MUDA WA KAZI ZIWASILISHE MAOMBI KWA KATIBU MKUU UTUMISHI YAKIAINISHA WATUMISHI WANAOHITAJI HUDUMA HIYO NA SABABU ZA MAHITAJI.

**IMETOLEWA NA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KILINDI.**